# UQAB

Jarida la

*Toleo 29 - Ramadhani 1440 H / Juni 2019 Miladi*




**Vipi Khilafah Itatatua Umasikini**

**Vipi Khilafah Itakavyo Waondolea Watu Mzigo wa Ushuru**

**Vipi Khilafah Itakavyo Andaa Jeshi Lenye Nguvu Duniani**

**Vipi Khilafah Italinda Uislamu na Ummah wa Kiislamu**

**Vipi Khilafah Itakavyo Sitisha Ukoloni ndani ya Ardhi za Waislamu**



## Hatua za Kivitendo Zitakazo Chukuliwa na Khilafah Rashida ili Kuzuia Ukosefu wa Ajira


uqab.or.ke

uqab_htk

UQAB-Magazine-1911964012162253

# Hatua za Kivitendo Zitakazo Chukuliwa na Khilafah Rashida ili Kuzuia Ukosefu wa Ajira

Ukosefu wa ajira ni mfano wa kadhia na matatizo mengineyo yaliyo sababishwa na mfumo huu wakilafi wa kiulimwengu wa kirasilimali, ikiwemo nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali inayotabikishwa ambayo huzalisha tu migogoro na majanga ya kiuchumi pekee, kwa kuwa iliunda nidhamu ya matabaka katika mujtama na kuongeza idadi ya wasiokuwa na ajira na kufilisi akiba za watu na kusambaratisha uchumi wa nchi nyingi duniani.

**Ukosefu wa ajira ni nini na ni lipi suluhisho linalohitajika kuutatua?**

Ukosefu wa ajira wamaanisha mtu kukosa uwezo wa kupata pato la kuendesha maisha ili kujipa kiwango stahiki cha maisha kwake. Maisha haya stahiki yanajumuisha mahitaji msingi ya chakula, nyumba na mavazi. Suluhisho la tatizo hili la ukosefu wa ajira lapaswa kuwa la kimsingi kuliko kuwa la kiviraka. Uhalisia wa maisha na maafa mabaya ya kiuchumi yamethibitisha kuwa hatua zilizo chukuliwa na madola ni za haraka, za muda na zenye mipaka. Muundo wa uchumi wa kirasilimali pamoja na benki zilizojengwa juu ya riba na kufungamanishwa na taasisi za kifedha, mikopo na ufichaji mali na noti za benki za lazima, ndiyo yanayojaza na kuongeza viwango vya ukosefu wa ajira licha ya madai ya kupungua kwake yakirudiwa rudiwa.

Suluhisho msingi la ukosefu wa ajira litakuwa kamilifu pekee katika nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu iliyojengwa juu ya misingi ifuatayo:

1- Utekelezwaji wa mfumo wa dhahabu na fedha badala ya mfumo wa noti za karatasi za lazima
2- Uharamishaji wa riba juu ya mikopo
3- Uharamishaji wa ufichaji mali

- **Mfumo wa pesa za karatasi za lazima:** Dola huendesha soko kwa kupitia kubuni migogoro iliyozaliwa na mfumo wa pesa za lazima, kama mfumko wa bei na nishati duni ya ununuzi na mporomoko wa kiuchumi na ufutaji wafanyikazi na waajiriwa ili kutatua kadhia hizi, kupitia moja ya suluhisho mbili:

* Kupitia uchapishaji pesa mpya endapo dola iko imara na pesa yake inatawala, basi itaijaza sokoni ili kuusukuma uchumi, na hili ndilo ambalo aliyekuwa Raisi wa Amerika Obama alilolifanya wakati wa mgogoro wa kiuchumi. Alichapisha mabilioni ya pesa za makaratasi ili kuongeza nishati ya ununuzi ya watu. Lakini wamiliki wa makampuni walishughulika na kugawanya bidhaa zao walizo zihifadhi na bidhaa zao ambazo hazijatumika wakati wa mporomoko wa kiuchumi, kabla ya uzalishaji wa bidhaa mpya, ambao wahitaji wafanyikazi wapya. Mpangilio huu sio suluhisho la tatizo la ukosefu wa ajira, bali ni suluhisho la uondoshaji bidhaa ambazo hazijatumika kabla ya oparesheni ya gurudumu la uzalishaji.

* Au dola iombe pesa kupitia uuzaji wa bondi na kuchukua mikopo kutoka kwa IMF na Benki ya Dunia. Hii ndiyo hali ya biladi nyingi za Kiislamu ambazo huanza kutoa ahadi baada ya ahadi ya utafiti ili kuzalisha uwekezaji mwingi ili kuuendesha uchumi na kufungua fursa mpya za kazi kwa mujibu wa madai yao. Lakini, "dawa hizi za kuondoa maumivu" hazitoki nje ya muundo wa kuongeza hazina za benki za riba na kampuni za hisa pasi na mbinu hii ya kuongeza mfumko wa bei sokoni kupewa umuhimu wowote.

Suluhisho linalopeanwa kupitia mfumo wa dhahabu na fedha katika tukio la mporomoko wa kiuchumi sio kuwafuta wafanyikazi na waajiriwa kama ilivyo katika mgogoro wowote wa kiuchumi katika mfumo wa kirasilimali, bali suluhisho ni kupunguza gharama ya uzalishaji, ikiwemo gharama za mishahara, na suluhisho hili halipelekei kifo cha gurudumu la uchumi wala ubadilishanaji wa mgogoro mmoja hadi mwengine, bali kinyume chake litaendelea hata kama ni pole pole. (Utapata ufafanuzi wa kina wa manufaa ya nidhamu ya dhahabu na fedha katika uchumi katika kitabu "Nidhamu ya Kiuchumi katika Uislamu" uk. 270 (Kiarabu))

- **Uharamishaji riba juu ya mikopo,** benki za riba ni muhimu katika nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali, kwani riba imekuwa ndiyo msingi wa biashara, ukulima na viwanda. Mikataba baina ya wakopeshaji na mabenki ni mikataba ya riba kwa sababu yanauza pesa kwa pesa, na kwa sababu yanazipatiliza juhudi za watu kwa riba iliyo lazimishwa pasi na kuanikwa katika aina yoyote ya hasara. Katika nidhamu ya kiuchumi ya Uislamu, Bait ul Mal hukopesha pesa ziso riba, baada ya kuangalia uwezekano wa kutumia pesa. Anayetaka kukopa huzihitaji imma kukimu maisha, au kwa ajili ya ukulima. Ama kwa hitajio la kwanza, Uislamu umedhamini hili kupitia kumhakikishia kila raia wa dola haki ya kuishi. Hitajio la pili limetimizwa na Uislamu kupitia kukopesha pesa kwa wahitaji bila ya riba. Omar ibn al-Khattab (ra) aliwapa wakulima pesa za kutosha nchini Iraq kutoka kwa Bait ul Mal, hadi ardhi zao zianze kuzalisha. Watalinganishwa na wakulima kama wao, wanaohitaji pesa, ili kujitosheleza kimaisha. Mtume (saw) alimpa mtu kamba na shoka ili akakate kuni na kuziuza ili ajikimu kimaisha.

- **Uharamishaji wa ufichaji mali,** pesa zilizozuiwa na wamiliki matajiri wa uchumi wa kirasilimali zilipelekea kujiondoa katika soko na kusitisha mzunguko mikononi mwa watu, ambao unapelekea upungufu wa uzalishaji wao kwa sababu hitajio la bidhaa limepungua na kusimamisha gurudumu la uchumi na hili hueneza ukosefu wa ajira katika mujtama kutokana na uchache wa mapato mikononi mwa watu. Katika nidhamu ya kiuchumi ya Uislamu, ufichaji mali umeharamishwa; pesa ni ala ya ubadilishanaji baina ya pesa kwa pesa, baina ya pesa kwa juhudi, na baina ya juhudi kwa juhudi. Kipimo hiki cha ubadilishanaji na maadamu ala hii inapatikana kwa watu, hii itasukuma kazi mbele na itaruhusu watu katika mujtama na matumizi yao jumla yatakuwa katika muundo wa duara la kuendelea linalo endeleza utajiri wa kiuchumi wa mtu binafsi na jamii. (Kwa kuwepo haja ya kusoma kuwa kuna tofauti kubwa kati ya ufichaji na akiba, utapata ufafanuzi katika kitabu "Nidhamu ya kiuchumi katika Uislamu" uk. 251 (Kiarabu). Kifungu cha 142 cha Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah: "Ufichaji mali umeharamishwa hata kama Zakah inatolewa."

***Endelea Uk..3***



Email: info@uqab.or.ke

Hizi ni baadhi ya suluhisho msingi ambayo nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu imeziweka sio tu kuondoa ukosefu wa ajira lakini pia kumaliza aina zote za ufisadi na utawala wa sera za kiuchumi za kirasilimali juu ya nchi.

**Ni mbinu zipi na hatua zipi za kivitendo zitakazo chukuliwa na Khilafah Rashida ili kuzuia ukosefu wa ajira?**

1- Kutafuta usawa wa kiuchumi kupitia kuwapa raia mafukara pekee wa dola mali za dola katika Bait ul Mal ambazo si katika zilizo kusanywa kutoka kwa Waislamu, bali kutoka katika mali ya ngawira hadi kupatikane usawa wa kiuchumi katika utoaji huu. Pindi Mtume (saw) alipoona mianya katika umilikaji wa mali baina ya Muhajireen na Answar, yeye (saw) aliwagawanyia pesa za ngawira (Fai') Muhajireen pekee, ambazo yeye (saw) alizipata kutoka kwa Bani An-Nadhir, ili kutafuta usawa wa kiuchumi. Imesimuliwa kuwa pindi Mtume (saw) aliposhinda kwa amani dhidi ya Bani al-Nadhir, na Mayahudi hao kufurushwa, Waislamu walimuomba Mtume (saw) kuwagawanyia (ngawira) baina yao. Aya ikateremshwa:

**...وَمَا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ مِنْهُمْ فَمَا أَوْجَفْتُمْ عَلَيْهِ**

"Na mali aliyo leta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwao hamkuyakimbilia mbio [hamkuyapata kwa kupigana]" [Al-Hashr: 6]

Mwenyezi Mungu (swt) ameufanya ugawanyaji uwe mikononi mwa Mtume (saw)
Aligawanya miongoni mwa Muhajireen, na hakuwapa Maanswari chochote isipokuwa wanaume wawili. Walikuwa mithili ya Muhajireen katika ufukara.

2- Mpangilio mpya wa mali ya Ummah ambayo ni ruhusa ya Mtungaji sheria kwa kundi kushiriki pamoja katika utumizi wa mali hiyo (ya Ummah). Na vitu vilivyo fafanuliwa kuwa mali ya Ummah ni vitu ambavyo Mtungaji sheria amevitaja kama vile vinavyotumiwa kwa ushirika na kundi, na kuwazuia watu binafsi kutokana na kuvimiliki peke yao na ni aina tatu:

(A) Huduma za jamii, kiasi ya kuwa ikiwa hazitapatikana katika mji au kikundi watatoka nje kwenda kuzitafuta, kama maji, malisho, huduma za jamii, nk.
(B) Madini yasiyo malizika.
(C) Vitu ambavyo kimaumbile haviwezi kumilikiwa na watu binafsi, kama barabara, mito, maziwa, bahari, shule za dola, mahospitali, nk.

Kifungu cha 140 cha Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah: "**Kila mtu miongoni mwa Ummah ana haki ya kutumia chochote katika mali ya Ummah, na hairuhusiwi kwa Dola kumruhusu mtu kumiliki au kuitumia kibinafsi.**" (Ili kuregelea hukmu za mali ya Ummah na kunufaika kutokana nazo soma Kielelezo hicho cha Katiba na Dalili zake Muhimu kuanzia Kifungu cha 137 hadi Kifungu cha 140)

3- Uislamu umefanya utoaji mahitaji kwa Ummah kuwa jukumu la dola kwa sababu Ummah una haki ya kusimamiwa. Dola inajukumu la utoaji mali na huduma kwa raia ikiongezewa na ugavi wa mali hii kwa wanajamii wote ili kila mmoja aimiliki na kuitumia. Bukhari amesimulia kuwa Ibn Umar (ra) amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: «الإِمَامُ الَّذِي عَلَى النَّاسِ رَاعٍ وَهُوَ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ» "Imamu aliye juu ya watu ni mchungaji na yeye ni mwenye kuulizwa juu ya raia wake."

Hii ni kinyume na yale tunayoyaona leo. Mnamo 2018, utajiri ulimwenguni ulikusanyika mikononi mwa mabilionea 26, ambao ni sawa na ule unaomilikiwa na wanadamu waliosalia!! Kifungu cha 124 cha Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah: **"Tatizo msingi la kiuchumi ni ugavi wa mali na manufaa kwa raia wote wa dola, na kusahilisha utumizi wao wa mali hii na kunufaika kwayo kupitia kuwawezesha kufanya bidii kwayo na kuimilki."**

4- Mtungaji sheria mwingi wa hekima aliwajibisha juu ya mwanamume mwenye uwezo kufanya kazi na kutoa mahitaji msingi (nafaqa) kwa nafsi yake na wale alio na majukumu juu yao. Mtoto mchanga ni wajib kupewa nafaqa, na ikiwa mrathi wake hawezi kufanya kazi, jukumu linaanguka kwa Bait ul Mal endapo hakutakuwa na mtu yeyote aliye na jukumu la utoaji nafaqa yao. Uislamu umeufanya usaidizi kwa mtu mlemavu au anayechukua hukmu ya mlemavu kuwa wajib juu ya Dola kwa mujibu wa Kifungu cha 153 cha Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah: **"Dola hudhamini ubunifu wa nafasi za kazi kwa wale wote wanaobeba uraia wake"**.

5- Ushajiishaji wa kuhuisha ardhi ya ukulima. Ukosefu wa ajira huondolewa kupitia ajira kwa masikini walio na uwezo wa kulima. Dola hugawanya ardhi zilizokufa kwa wale wasiomiliki ardhi au wanaomiliki sehemu ndogo. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alimpa Bilal Al Muzni ardhi baina ya bahari na jabali. (Ili kuregelea sheria za ugavi wa ardhi zilizokufa na kuzihuisha – Kifungu cha 134, 135, 136 vya Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah).

6- Dola kuanzisha vituo na taasisi za utafiti wa sayansi ya kiteknolojia, hususan kwa kuwa sera ya viwanda imefungika kikamilifu na teknolojia. Endapo dola itawakumbatia wanasayansi na wenye vipaji na kuwapa maisha stahiki, tutaona uvumbuzi ukijitokeza baada ya kuzikwa au kuhama, na Waislamu watarudi pale wanapostahiki kuwa miongoni mwa mataifa katika viwango vyote vya kiuchumi, kisiasa, kijeshi na kithaqafa.

Na hadi ukosefu wa ajira utakapo kwisha na Waislamu kunufaika kutokana na rasilimali za biladi yao, na matatizo yote ya kiuchumi kutatuliwa, mageuzi ya kimsingi na mapinduzi ni lazima yapatikane, ili jambo hili lienee kila mahali, na jambo hili ni utawala wa Kiislamu, ili wanadamu wafurahie uadilifu, wema na uchungaji wa kisawa sawa kwa mujibu wa hukmu za kishari'ah, na Dola ya Khilafah Rashida iwe ndiyo muundo wa yale tunayowasilisha; Uislamu kama badala kwa urasilimali unaokufa, na Mwenyezi Mungu ifanye kurudi kwake iwe hivi karibuni.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Rana Mustafa**

# Vipi Khilafah Itatatua Umasikini: SEHEMU 1

• Licha ya rasilimali na nguvu kazi nyingi, pamoja na utajiri mkubwa kabisa wa mafuta duniani na hifadhi ya madini katika ardhi za Waislamu, wengi wa Ummah wa Waislamu wanateseka katika umasikini mkubwa, wakiwa na pato la chini ya dolari 1.9 za kimarekani kwa siku ili kukidhi mahitaji yao msingi. Ukosefu mkubwa wa ajira unaokua, uzorotaji wa ukulima na viwanda, ongezeko la ushuru, kupanda mara kwa mara kwa bei pamoja na gharama ya juu ya umeme na kudumu kukosekana kwake, ni ushahidi wazi wa usimamizi mbaya na ufujaji katika ardhi zetu na ugavi mkubwa wa kimakosa wa utajiri wetu. Uwekezaji wa serikali katika miundombinu na huduma za Ummah ili kushibisha mahitaji msingi ya watu ni mchache au haupo.

Kimsingi hizi ni najita ya sera zisizokuwa za Kiislamu kwa mujibu wa maelekezo ya ajenda za kisiasa za dola za kikoloni za kirasilimali zinazo tekelezwa na watawala ndani ya ardhi za Waislamu, ikiwemo mikopo ya IMF na Benki ya Dunia, inayo lazimisha sio tu viwango vya juu vya riba lakini pia sera haribifu za uchakachuaji uchumi ndani ya ardhi zetu Waislamu.

• Ukweli ni kuwa; ugavi wa kiusawa na wa kibinadamu wa utajiri ili kutoa mahitaji ya kila mtu sio miongoni mwa malengo ya uchumi wa kirasilimali. Fauka ya hayo, udumishaji mwanya mkubwa katika utajiri baina ya tajiri na masikini hunufaisha mfumo wa kirasilimali, kwa kuwa uwepo wake umejengwa juu ya utumiaji watu vibaya, na ukuzaji wa kipote kichache cha wamiliki rasilimali, wanaowakilisha, kudumisha, na kutawala kwa mfumo wa kirasilimali, na wale waliopagawishwa na nguvu za kimada wakiongezeka kila uchao. Hivyo basi ulafi, ushindani wa kidhulma, utumizi mbaya na muungozo wa kiuchumi wa "Samaki Mkubwa Humla Samaki Mdogo" umewanyima wanadamu haki zao na mahitaji yao msingi.

"Kwa mujibu wa shirika la msaada wa Oxfam, mabilionea wakubwa zaidi 26 wanamiliki rasilimali nyingi zaidi kuliko wanazomiliki watu bilioni 3.8 ambao ndiyo nusu ya idadi ya mafukara duniani. Utajiri wa asilimia 1 ya matajiri zaidi duniani ni sawa na utajiri jumla wa asilimia 99 waliosalia." "Takriban watu 10,000 kwa siku hufa kwa ukosefu wa matibabu na watoto milioni 262 hawako shuleni, kwa sababu wazazi wao hawawezi kumudu gharama ya karo, sare za shule au vitabu. Wanawake wanakufa kwa ukosefu wa huduma stahiki za uzazi na watoto wananyimwa elimu ambayo ingekuwa ndiyo njia yao ya kujitoa katika umasikini." (Ripoti ya Oxfam ya 2019: https://www.oxfam.org.nz/reports/public-good-or-private-wealth) Khilafah Haitazuia Tu Umasikini Pekee Bali Inalenga Kuimarisha Kiwango cha Maisha cha Kila Raia Wake!

• Kwanza; nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu imejengwa kwa msingi safi wa Qur'an na Sunnah pekee, inayotaka kutoka kwa mtu binafsi na dola kulinda mipaka ya Mwenyezi Mungu (swt). Uislamu unaikataa nadharia ya ongezeko la mahitaji ya wanadamu na uhaba wa rasilimali kama inavyo wasilishwa na urasilimali. Uislamu unaeleza waziwazi kuwa Mwenyezi Mungu (swt) ameumba rasilimali za kutosha ili kukidhi mahitaji ya kila mtu.

وَسَخَّرَ لَكُم مَّا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مِّنْهُ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

"Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika haya zimo ishara kwa wale watu wanaofikiri." [Al-Jathiyah: 13]

• Mtume wetu Muhammad (saw) amesema yafuatayo kuhusiana na mahitaji msingi ya mtu binafsi:

لَيْسَ لِابْنِ آدَمَ حَقٌّ فِي سِوَى هَذِهِ الْخِصَالِ بَيْتٌ يَسْكُنُهُ وَثَوْبٌ يُوَارِي عَوْرَتَهُ وَجِلْفُ الْخُبْزِ وَالْمَاءِ

"Mwanadamu hana haki zaidi kuliko mambo haya; nyumba anayoishi, na nguo anazostiri uchi wake, na kipande cha mkate na maji." [Tirmidhi]

Hizi ndizo haki ambazo Uislamu unamhakikishia kila mtu na hizi ndizo haki ambazo urasilimali umewanyima wanadamu… Mwenyezi Mungu (swt) ameufanya kuwa wajib juu ya Khilafah kumsahilishia kila mtu kuweza kushibisha mahitaji yake msingi. Dola yapaswa kuhakikisha kuwa mja wa Mwenyezi Mungu anaweza kutimiza jukumu lake la utafutaji riziki, na kufanya juhudi za kuchuma riziki. Mwanamume mwenye uwezo ana jukumu la kufanya kazi ili kushibisha mahitaji yake mwenyewe. Ama kwa wanawake, na wale wanaume ambao hawana uwezo wa kufanya kazi, ni jukumu kuwapa masrufu yao na hii ni haki kwao, na Dola inawajibika kuwapa mahitaji yao endapo wasimamizi wao wa kiume hawana uwezo wa kufanya hivyo. Zaidi ya hayo, kutoa masrufu kwa mke ni jukumu juu ya mume. Kutoa masrufu juu ya watoto ni jukumu juu ya baba.

(وَعَلَى ٱلْمَوْلُودِ لَهُ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِٱلْمَعْرُوفِ) "Na juu ya baba yake chakula cha kina mama, na nguo zao kwa mujibu wa ada." [Al-Baqara: 233]

Mtume (saw) amesema:
«كَفَى بِالْمَرْءِ إِثْمًا أَنْ يُضَيِّعَ مَنْ يَقُوتُ» "Yatosheleza kuwa ni kosa kwa mume kumtelekeza aliye chini ya usimamizi wake." (Abu Dawud, Al-Nawawi) Hii yamaanisha kuwa kazi ni wajib juu ya huyu mwanamume aliye na uwezo na endapo hatafanya kazi ataadhibiwa kama ilivyo hali kwa kila jukumu.

Kunapokosekana yeyote aliye wajibishwa kulipia masrufu, au endapo watakuwepo lakini hawana uwezo wa kulipia masrufu hayo, Shari'ah imewajibisha masrufu haya juu ya Bait al-Mal (Hazina ya Dola), kwa maana nyengine, juu ya Dola ya Khilafah. Kwani Rasulullah (saw) amesema:

أَنَا أَوْلَى بِالْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنْفُسِهِمْ مَنْ تَرَكَ مَالاً فَلأَهْلِهِ وَمَنْ تَرَكَ دَيْنًا أَوْ ضَيَاعًا فَإِلَيَّ وَعَلَيَّ

"Mimi ni bora kwa waumini kuliko nafsi zao. Yeyote anayeacha mali, basi ni ya watu wake, na anayeacha deni, au wanaomtegemea basi hilo ni langu na juu yangu," (imeripotiwa na Muslim kutoka kwa Jabir)

Hii pia ni dalili kuwa miongoni mwa kadhia muhimu zaidi kwa Khilafah ni kusimamia mambo ya Ummah au kubuni nafasi za kazi kwa wale walio na uwezo wa kufanya kazi lakini hawana kazi.

• Ushibishaji wa Mahitaji yasiyo msingi Mahitaji ya Ziada ni lazima pia usahilishwe na Khilafah, katika njia ile ile kama katika mahitaji msingi. Dola huwarahisishia raia wote ili kuweza kushibisha mahitaji yao ya ziada (yasiyo msingi), na kuleta usawa katika mujtama kwa njia ifuatayo:

a) Kupitia kuwapa rasilimali taslimu na ziso taslimu kutoka katika fedha za Bait al-Mal, na kutoka katika ngawira za kivita, na chengine chochote mfano wa haya.
b) Kuwagawanyia baadhi ya ardhi yake ya ukulima wale wasiokuwa na ardhi ya kutosha. Wale wanaomiliki ardhi

*Endelea Uk..5*

lakini hawaitumii hawapewi zaidi. Wale wasiokuwa na uwezo wa kulima ardhi zao wanapewa usaidizi wa kifedha ili kuwawezesha kuzilima.
c) Kuwapa usaidizi wale wasiokuwa na uwezo wa kulipa madeni yao kupitia kuwapa pesa za Zakah, na ngawira za kivita, na chengine chochote mfano wa haya.

Hizi ni aina zote za usaidizi ambazo hatuwezi kuzipata chini ya serikali za kirasilimali katika ardhi zetu.

• Usalama, aina zote za huduma za Ummah kama huduma za afya na elimu, ni jukumu linalopaswa kutekelezwa na Khilafah, ikiongezewa na kuhakikisha mahitaji ya watu binafsi. Haya hayana budi kufadhiliwa na hazina ya Dola (Bait al-Mal) kwa kila raia wake, bila ya kujali dini zao, rangi, jinsia au kabila.

Inapaswa kuzingatiwa kuwa ukosefu wa usalama hupelekea kushindwa kutimiza majukumu mengine yote. Hiyo ndiyo sababu ahadi ya mwanzo kabisa ya Rasulullah (saw) aliyowapa maswahaba zake, pindi alipowajuza kuhusu Hijrah, ilikuwa ni usalama:

إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ جَعَلَ لَكُمْ إِخْوَاناً وَدَاراً تَأْمَنُونَ بِهَا

“Allah Azza wa Jalla amewajaalieni kuwa ndugu na ardhi ambamo munapata amani ndani yake.” [Sirah, Ibn Ishaq]
Kutokana na hayo, masalihi na huduma za Ummah ni lazima zitekelezwe na Dola ya Khilafah, kwa mujibu wa maneno ya Rasulullah (saw):
«الإِمَامُ رَاعٍ وَهُوَ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ» “Imamu (mtawala) ni mchungaji, na yeye ataulizwa kuhusu raia wake.” (imeripotiwa na Al-Bukhari kutoka kwa Abdullah Bin Umar).

• Nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu hairuhusu ulimbikizaji wa mali mikononi mwa wachache. Hivyo basi, wakati wowote kunapotokea mwanya, Khalifah ni lazima afanye kazi kuleta usawa kupitia kuitekeleza kivitendo aya hii:

كَيْ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْاَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ

“Ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu.” [Al-Hashr: 7]

• Uislamu kwa ujumla umeharamisha ufichaji utajiri na kufaradhisha Zakah, ili kuhakikisha kuwa utajiri unagawanywa miongoni mwa watu. Mwenyezi Mungu (swt) anaonya katika jambo hili:

وَٱلَّذِينَ يَكْنِزُونَ ٱلذَّهَبَ وَٱلْفِضَّةَ وَلَا يُنفِقُونَهَا فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ

“Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie habari ya adhabu iliyo chungu.” [At-Tawbah: 34]

• Tunayokumbana nayo ya usimamizi mbaya na ukosefu wa miundombinu hayata kuwepo chini ya Khilafah. Chini ya Khilafah, Uislamu utaachilia kiwango kikubwa cha kipekee cha pesa katika uchumi na kuimarisha kilimo na maendeleo ya kiviwanda, pasi na kuongeza ushuru, kupitia uundaji upya wa kimsingi wa muundo wa dola, umilikaji wa Ummah na wa kibinafsi miongoni mwa hatua nyenginezo.

• Uislamu unawajibisha kuundwa kwa msingi imara wa viwanda vizito, ukisaidiwa kupitia utafiti unaoongoza wa kiulimwengu, ili kusukuma mbele Khilafah katika dori yake kama dola inayoongoza. Ukulima chini ya Khilafah ulikuwa ukionewa wivu ulimwenguni kwa karne nyingi na utaonewa tena wivu! Kwani Uislamu utaunganisha umilikaji wa ardhi pamoja na ulimaji wake wa kivitendo, utaondoa umilikaji wa kigeni wa ardhi ya ukulima, pamoja na utozaji mzito wa ushuru juu ya pembejeo za ukulima. Huu utakuwa ni utiaji nguvu usalama wa chakula pamoja na ufanisi wa kindani kama Ummah walivyofurahia kwa karne nyingi chini ya utawala wa Kiislamu. Hivyo basi leo Khilafah itayapa kipaumbele mazao yanayo waruhusu raia wake kupata mahitaji yao msingi ya chakula na mavazi kikamilifu, huku uzalishaji wa ziada ukitumiwa kwa ajili ya biashara ya kigeni. Itabuni maeneo thabiti ya malisho ili kusaidia ongezeko la uwepo wa mifugo.

• Kwa sasa, umeme, makaa ya mawe, mafuta na gesi ya kimaumbile ni ghali na mara nyingi havipatikani kutokana na kubinafsishwa na warasilimali. Khilafah itaondoa umilikaji wa kibinafsi wa rasilimali za kawi na kuziregesha katika umilikaji wa Ummah ili nishati ipeanwe kwa usahali na vile vile kwa urahisi. Itaondoa ushuru juu ya nishati na mafuta ambao umefumua zaidi bei zake. Hivyo basi Khilafah itaonyesha ukweli wa Dini ya Uislamu kivitendo kwa ulimwengu uliosambaratishwa kutokana na mfumo fisadi wa urasilimali ambao unaporomoka.

• Mojawapo ya ala za ukandamizaji mbaya zaidi wa uchumi wa kirasilimali ni utozaji ushuru! Ambapo ndani ya Khilafah, hakuna ushuru wa mapato wala ushuru wa mauzo, kwa sababu mali ya mtu binafsi kiasili ni haramu kuchukuliwa pasi na haki. Utozaji ushuru hufanywa kwa utajiri wa ziada fauka ya unaohitajika kushibisha mahitaji msingi na hili pia liko chini ya masharti makali. Kinachoruhusu sera hii ya utozaji wa chini wa ushuru ni kule kuwa Khilafah ina vyanzo vya kutosha vya mapato kutoka katika mali ya Ummah na Dola, pamoja na mkusanyiko wa hukmu za kipekee za uzalishaji mapato kutoka katika ukulima na viwanda.

• Baada ya kuunyima Ummah mapato yake stahiki na pia kuyanyonga machumo yake na uwezo wa kununua na kuzalisha, serikali vibaraka katika ardhi zetu zimechukua mikopo ya riba kutoka katika nchi za kikoloni za kikafiri. Mikopo hii ni mtego wa kinyama, ulioundwa ili kuzidumisha ardhi za Waislamu ndani ya mikopo, kuzipokonya rasilimali zetu, na kupunguza pakubwa uwezo wetu wa kusimama kwa miguu yetu kupambana na Magharibi.

• Ongezeko la mara kwa mara la mfumko wa bei katika ardhi zetu ni kutokana na pesa zinazo pungua thamani yake daima, kwa kuwa hazikujengwa juu ya dhahabu na fedha kama inavyo wajibishwa na Shari’ah. Pesa za dola zitaasisiwa tena juu ya kipimo cha dhahabu na fedha ambacho ndiyo ngome ya kweli ya kuondoa mfumko wa bei kwa mzizi wake. Khilafah itatoa pesa yake huru, iliyofungwa kwa dhahabu na fedha, na haitafungamanishwa kwa pesa yoyote ya kigeni kwa njia yoyote ile. Khilafah haitachukua mikopo yoyote ya riba kutoka katika nchi za kikoloni za kikafiri.

• Khilafah itarudisha tena ardhi zetu katika ufanisi na neema kama zilivyokuwa katika zama za nyuma chini ya utawala wa Uislamu. Maneno ya Rasulullah (saw) sio tu ni dalili ya majukumu na wajibu wa Khilafah, ni ahadi na bishara njema.
«الإِمَامُ رَاعٍ وَهُوَ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ» “Imamu ni mchungaji na yeye ni mwenye kuulizwa kuhusu raia wake”

• Afrika, kwa mfano, ilikuwa mbali kabisa na kuwa sehemu masikini na yenye njaa zaidi ya ulimwengu huu wakati wa zama za Khalifa Umar ibn Abdul Aziz, kwa sababu hakutekeleza chochote isipokuwa hukmu na qaida za Dini ya Uislamu.

Endelea Uk..6

Imesimuliwa na Yahya bin Said, aliyekuwa Wali wa wakati huo katika zama za utawala wa Khalifa Umar bin Abdulaziz (ra), kuwa alisema: "Nilitumwa na Umar bin Abdul Aziz kukusanya zaka kutoka Afrika. Baada ya kuzikusanya, nilidhamiria kuwapa masikini. Lakini, sikumpata yeyote. Umar bin Abdul Aziz amewafanya watu wote kuwa matajiri wakati wa zama zake. Hatimaye, niliamua kutumia hazina hiyo ya zaka kuwanunua na kuwaacha huru watumwa" Ibn Abd Hakam, Abdullah (1994) Al-Khalifat al-Adil Umar ibn Abd Aziz: Khamis al-Khulafa al-Rasyidin. Dar al-Fadilat, Kaherah 78

• Kwa hivyo yasadikisheni maneno ya Mwenyezi Mungu (swt), kwa sababu tayari muna imani kwayo, ili sisi kama Ummah na waliosalia ulimwenguni tufurahie matunda ya Uislamu haraka iwezekanavyo, inshaallah!

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اسْتَجِيبُواْ لِلّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُم لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُواْ أَنَّ اللّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ

"Enyi mulio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapokuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa." [Al-Anfal: 24]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Zehra Malik**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vipi Khilafah Itatatua Umasikini – SEHEMU 2

## Mifano ya Kivitendo kutoka katika Sunnah na Historia ya Kiislamu

• Kwanza kabisa ni kuanza kwa ukumbusho mfupi wa nguzo kuu za Uislamu katika kuzuia umasikini:

- Uislamu umeidhibiti kadhia ya umilikaji katika njia wazi na thabiti. Kila mtu binafsi anaruhusiwa kupata na kumiliki mali ya kibinafsi juu ya kila kitu ambacho si mali ya Ummah au Dola, kupitia njia ambazo Uislamu umeziruhusu (kazi, biashara, urathi, zawadi, nk.), yaani isipokuwa wizi, ulaghai, rushwa, kamari na riba, ufichaji mali …

- Uislamu umeharamisha ufichaji mali, unaoitwa kanz (ufichaji dhahabu na fedha, hata kama Zakah inalipwa juu yake), na ufichaji wa chakula, Ukiritimba, unaoitwa ihtikar. Huku ni kuzuia, kuficha bidhaa, kwa matarajio ya kuongezeka kwa bei. Nususi za kiShari'ah na fiqh zafafanua waziwazi kitendo hiki kuwa ni haramu. Kuna riwaya kadha wa kadha kutoka kwa Rasulullah (saw) zinazo elezea waziwazi kuwa ihtikar ni haramu … Said ibn Al-Musayyib amesimulia kutoka kwa Mu'ammar ibn Abdullah Al-'Adawi katika Bukhari kuwa Mtume (saw) amesema: «لاَ يَحْتَكِرُ إِلاَّ خَاطِئٌ»"Hafanyi ukiritimba isipokuwa mkosefu." Al-Athram amesimulia kutoka kwa Abu Umamah, amesema: «نَهَى رَسُولُ اللهِ ﷺ أَنْ يُحْتَكَرَ الطَّعَامُ» "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amekataza ukiritimba wa chakula". Na Muslim amesimulia kupitia silsila yake ya wasimulizi kutoka kwa Said ibn Al-Musayyib kuwa Mu'ammar alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: «مَنِ احْتَكَرَ فَهُوَ خَاطِئٌ» "Mwenye kufanya ukiritimba basi yeye ni mkosaji." Ukiritimba umeharamishwa katika vitu vyote pasi na tofauti kati ya vyakula au vyakula vya wanyama, vyakula au visivyo vyakula, na katika mahitaji msingi ya watu au ya ziada. Hivyo mwenye kufanya ukiritimba kiuhalisia huwa anataka kuongeza bei kiuadui kwa ajili ya kuwafanyia uadui Waislamu, jambo ambalo ni haramu, kutokana na yale yaliyo simuliwa kutoka kwa Ma'akal ibn Yasar, kuwa alisema kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: «مَنْ دَخَلَ فِي شَيْءٍ مِنْ أَسْعَارِ الْمُسْلِمِينَ، لِيُغْلِيَهُ عَلَيْهِمْ، كَانَ حَقّاً عَلَى اللهِ أَنْ يُقْعِدَهُ بِعُظْمٍ مِنَ النَّارِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ» "Yeyote anayetia chochote katika bei za Waislamu, ili kuwaongezea, itakuwa ni haki juu ya Mwenyezi Mungu kumtia Motoni kwa uadui Siku ya Kiyama."

- Uislamu umeharamisha kampuni na biashara za hisa. Ushirika na biashara ni lazima zijengwe juu ya ushirikiano halisi baina ya watu binafsi kwa msingi wa pesa + juhudi na/au ujuzi, huku bidhaa ya ushirikiano au biashara ni lazima iwe bidhaa halisi yenye thamani halisi.

- Na Uislamu umefanya dhahabu na fedha kuwa sarafu pekee ya dola na umeifanya kuwa huru na sarafu nyengine yoyote au dola au makubaliano ya kimataifa.

- Hakuna riba katika sehemu yoyote ya uchumi iwe kwa watu binafsi au Dola. Benki iliyopo pekee ni benki ya dola, inayotoa mikopo bila ya riba yoyote. Na Dola hairuhusiwi kuchukua mikopo kutoka kwa dola nyenginezo kwa msingi wa riba.

- Hakuna ushuru katika Uislamu. Khilafah haito na haipaswi kuchukua ushuru kutoka kwa watu …

Umasikini uliopo katika ardhi zetu na kote ulimwenguni unasababishwa na ukosefu wa hukmu hizi! Hivyo ikiwa hukmu zote hizi zitatabikishwa hakuna sababu itakayo bakia ambayo huenda ikapelekea kutokea au kuongezeka kwa umasikini ndani ya Dola. Hivyo basi, Khilafah ina mbinu fulani za kugawanya utajiri miongoni mwa watu, bila ya kujali dini zao, rangi au jinsia. Ni lazima tutambue kuwa haitawezekana, au kwa ufupi haiwezekani, kutabikisha siasa hizi za Kiislamu chini ya nidhamu zisizo kuwa za Kiislamu zilizoko leo.

* Kwanza kabisa, Uislamu unazalisha kazi, unasahilisha ajira na hautilii maanani upungufu wa nafasi za kazi/ufutaji kazi kama chombo cha kiuchumi kama ilivyo katika urasilimali. Urasilimali huzingatia upunguzaji wa nafasi za kazi na hivyo basi kiwango fulani cha ukosefu wa ajira kama njia ya kuhifadhi mtaji wa wenye mtaji. Kwa haya, dola itamshajiisha kila mwanamume, aliye na uwezo wa kufanya kazi, kutafuta kazi au kutafuta njia za kupata mapato ili kukidhi mahitaji yake, na mahitaji ya walio chini ya jukumu lake, kama mkewe, watoto, dada zake na wazazi. Usimamizi wa kifedha hulazimishwa juu ya mume kwa mkewe, watoto kwa baba yao, wazazi wawili kwa watoto wao wa kiume, na mrathi juu ya jamaa zake. Yote haya yamedhibitiwa kupitia nususi wazi za kiShari'ah. Uislamu umedhamini mahitaji msingi yaliyo tajwa kwa raia wote wa dola kupitia usimamizi wa kifedha, isipokuwa katika hali mbili: ya kwanza endapo mtu hana mrathi, pili endapo mtu aliye kalifishiwa usimamizi hana uwezo wa kutoa. Katika hali hii usimamizi utakalifishiwa Hazina ya Dola (Bait ul-Mal), kama alivyosema Mtume (saw): «مَنْ تَرَكَ كَلّاً فَإِلَيْنَا وَمَنْ تَرَكَ مَالاً فَلِوَرَثَتِهِ» "Yeyote aliye wacha kallan basi ni jukumu juu yetu na yeyote aliye wacha mali basi ni ya warathi wake" (Kall ni mtu dhaifu asiyekuwa na mtoto wala baba).

*Endelea Uk..7*

•* Dola katika Uislamu pia hudhamini mahitaji msingi ya raia wake wote, ambayo ni: usalama, matibabu na elimu, kwa mujibu wa nususi husika za kisheria, na kwa namna iliyo tangulia. Inapaswa kuzingatiwa kuwa mapato ya Bait ul-mal aghlabu huwa yanatosheleza kukidhi mahitaji haya pasi na kutoza ushuru juu ya Waislamu matajiri kwa ajili yake. Endapo lakini mapato ya kudumu ya Bait ul-Mal yatakuwa hayatoshelezi mahitaji hayo, ushuru hutozwa Waislamu matajiri ili kukidhi yanayo hitajika. Sheikh Ata' bin Khalil Abu Al-Rashtah, Migogoro ya Kiuchumi: Uhakika Wake na Suluhisho kutoka katika Mtazamo wa Uislamu)
Kutokana na hayo, ikiwa tunakumbuka mfano wetu kutoka Sehemu ya 1 ya Makala haya, unaoeleza kuwa wakati wa Umar (ra) dola haikumpata yeyote wa kumgawanyia Zakah barani "Afrika", huu hapa ndiyo ufafanuzi wake wa ni kwa nini Zakah hii haikuweza kugawanywa! … Alhamdulillah …

•* Uchumi wa Kiislamu unaweza kufanya kazi pekee ndani ya utabikishaji kamilifu wa kila utawala na nidhamu ya Kiislamu. Hivyo basi hitajio msingi zaidi lilikuwa na litakuwa ni uwepo wa Khilafah, na kiongozi wake mcha Mungu, Khalifah. Historia imejaa shakhsiya za watu zisizokuwa na idadi, walio watawala watu wao juu ya Taqwa, lakini Khalifah Omar bin al-Khattab (ra) amewacha mifano mingi zaidi na inayong'aa ya ni zipi sifa ambazo mtawala huyu anapaswa kuzimiliki. Uislamu umetoa malengo na sheria kwa ajili ya kutabikishwa nidhamu ya kisiasa na kiuchumi zenye kujali.

•* Khalifah Omar ibn Khattab (ra) alikuwa ndiye Khalifah wa mwanzo kubuni muundo msingi wa sera ya kijamii iliyo na taasisi na muundo kwa mujibu wa majukumu na mahitaji kutoka katika Qur'an na Sunnah, iliyowarahisishia Makhalifah waliofuata kutimiza majukumu yao kama wachungaji na wasimamizi wa watu ndani ya Dola ya Kiislamu ya Khilafah. Aliweka utaratibu wa huduma za Ummah na nidhamu ya kuangalia maslahi ya masikini na mafukara. Alikuwa wa kwanza kuweka taasisi za Manufaa kwa watoto, mayatima, wajane na walemavu, vile vile mafao kwa wazee, marupurupu kwa wasio na ajira na hata huduma za matibabu ya Ummah… Na hata masikini miongoni mwa Mayahudi na Manaswara katika ardhi zilizo funguliwa, ambao Uislamu uliwakadiria kama raia kamili wa Dola, walipokea malipo kutoka kwa Bait ul-Mal. Wale waliofanya ukiritimba, au kuzuia bidhaa msingi kwa lengo la kuongeza bei waliadhibiwa kwa njia tofauti tofauti, ikiwemo kufukuzwa nchi hadi ardhi nyenginezo.

•* Katika zama za utawala wote wa Makhalifah Waongofu (Khulafah u-Rashideen), KILA mtoto, hususan wale wanaohitajia msaada, walipokea manufaa kutoka kwa Bait ul-Mal. Umakinifu maalum ulipewa hususan usimamizi wa haki za kisheria, kielimu, na kifedha za watoto mayatima. Khalifah Umar (ra) kwa mfano, aliagiza walezi na wasimamizi wa watoto wasio na baba kuiongeza mali yao kupitia kuifanyia biashara ili kuiepusha kupunguzwa kupitia ulipaji Zakah. Alisema: "Ifanyieni biashara mali ya mayatima na hapo haitaliwa na Zakah." Na pindi mtu mmoja alipokuja kwake na mtoto aliyempata ametelekezwa, alimwambia mtu huyo: "Yuko huru, ulezi wake ni juu yako, na nafaqa yake ni jukumu letu na itatolewa na Bait ul-Mal." Khalifah Ali (ra) alitenga Dirham 10 kwa mtoto mchanga aliye telekezwa.

•* Pindi Umar (ra) alipo pokea zawadi ya tamu tamu kutoka kwa wali wake nchini Azerbaijan, alitaka kujua ikiwa watu wote huko wamekula tamu tamu hizo. Jibu lilikuwa zilitengewa mabwenyenye katika jamii. Umar (ra) kisha akatoa agizo lifuatalo kwa wali huyo: "Usijishibishe kutokana na chakula cha aina yoyote hadi Waislamu wote wale shibe yao kutokana nacho kabla yako."

•* Rasulullah (saw) aliyapa umakinifu maalum mahitaji ya wanawake wajane. Jukumu hili lilibebwa na Makhalifah kwa umakinifu na uchungaji huo huo. Abu Bakr (ra) alinunua nguo na kuzigawanya kwa wajane masikini wakati wa miezi ya baridi. Umar (ra) aliwalipa malipo ya kudumu wanawake, waliohama kutoka Makka hadi Madina. Ali (ra) aliendelea kutimiza jukumu hili kwa watu wote masikini, wajane, na watu wengineo waliohitaji – Malipo ya usaidizi!

•* Khalifah Umar (ra) mara kwa mara alimzuru na kumkidhia mahitaji mwanamke kipofu mjini Madina, aliyekuwa hana mtu wa kumkidhia mahitaji yake. – Manufaa ya Walemavu! Pia alitoa maagizo kuwa malipo yangeruhusiwa kwa ajili ya watoto wanao nyonyeshwa na baadaye kupanua hilo hadi kwa kila mtoto kuanzia siku anapozaliwa. Kiwango kilikuwa Dirham 100 kuanzia siku ya kuzaliwa, Dirham 200 anapo kua na hata zaidi anapo baleghe. Pia alitenga Dirham 6 zaidi kwa kila mtoto, wa kiume au wa kike, juu ya zile alizompa baba kwa usaidizi. Malipo haya yaliendelea chini ya makhalifah waliofuata – Manufaa ya Watoto! (http://dergipark.gov.tr/download/article-file/399406)
Taasisi maalumu ilibuniwa ili kusimamia mambo ya kisaikolojia, kijamii na kifedha ya familia za wanajeshi, hususan wanapokuwa hawako, au ulemavu kutokana na utekelezaji majukumu yao, au katika hali wanapouwawa mashahidi vitani, kwa mujibu wa mfano wa Rasulullah (saw).

•* Khalifah Umar (ra) alimwita mke wake mwenyewe kumsaidia kama mkunga mwanamke wa kibedui aliyekuwa na uchungu wa uzazi, huku yeye mwenyewe akiitayarishia chakula familia hiyo wakati huo mgumu. Wakati wote huo aliketi nje ya hema akisubiri kuzaliwa kwa mtoto. Siku iliyofuatia alitenga malipo ya kudumu kutoka kwa Bait ul-Mal kwa familia hiyo – Manufaa ya Uzazi na Nafaqa na Usaidizi!

Na hakutofautisha baina ya Muislamu na asiyekuwa Muislamu. Alimtumikia kila raia wake: Alitenga malipo ya kila siku kutoka katika Bait ul-Mal kwa Yahudi mmoja mzee masikini kwa kusema: "Wallahi, ni kinyume na ada ya uadilifu kuwa tuchukue Jizyah (kodi kwa Wasiokuwa Waislamu) kwao wanapokuwa vijana na wenye afya, na tuwaache pasi na uchungaji wanapokuwa wazee?" – Usaidizi wa Wazee / Mafao! Alikiona kikundi cha Manaswara wakiugua Ukoma, na hivyo kutumia kutoka katika Bait ul-Mal kuwatibu. – Huduma za Matibabu! Na wale, ambao hawatibiki, walipewa marupurupu ya kudumu hadi siku yao ya mwisho. – Manufaa ya Maradhi!

•* Khilafah Uthmaniyya ilichunguza na kufuatilia kila chakula kabla ya kutoa ruhusa ya kuuzwa sokoni. Ili kudhibiti bei wakati wa upungufu wa usambazaji katika maeneo fulani, Khalifah angeshajiisha ushindani kupitia uagizaji kutoka sehemu nyenginezo za Khilafah. Mfano mmoja ni wakati wa utawala wa Khalifah Abdul Hamid I (1774 – 1789). Wakati wa uhaba wa usambazaji wa nyama jijini Istanbul, ambapo wauza nyama walianza kuongeza bei za nyama, na hata kuacha kuiuza, aliwaamuru wauza nyama kutoka Thrace kuja na kufungua mabucha jijini Istanbul. Hivyo basi kupitia ongezeko la ushindani, bei zilishuka tena kwa kiwango cha kuweza kumudiwa. Khilafah pia ilitabikisha faini kwa mauzo maovu. Wale walio punja katika mizani walilazimika kulipa faini: sarafu 1 ya fedha (Akce) kwa gramu 5 za nyama iliyouzwa kimakosa.

*Endelea Uk..8*

Vifungu vya sheria vya wauza nyama pia vimeashiria kukamatwa kwa wauza nyama, ambao hawakutaka kuuza nyama. (http://dergipark.gov.tr/download/article-file/185222 na makala mengineyo tofauti tofauti ya historia)

Hii ni mifano michache tu ya namna Khilafah inavyo chunga mambo ya watu wake na kuchangamka katika kuchukua hatua thabiti katika vita dhidi ya umasikini. Mwenyezi Mungu (swt) aturuzuku siku hizi za baraka kwa kurudi Khilafah Rashidah kwa Njia ya Utume hivi karibuni mno bi'idhnillah!

لَا تَقْنَطُواْ مِن رَّحْمَةِ ٱللَّهِ

"…Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu"

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya H izb ut Tahrir na**

**Zehra Malik**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vipi Khilafah Itakavyo Waondolea Watu Mzigo wa Ushuru

• Ili kuendesha mambo ya dola na watu, kila dola inahitaji pesa. Chini ya urasilimali pesa hizi kimsingi hukusanywa kupitia riba na ushuru wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja. Vile vile katika Uislamu, Dola inapaswa kufadhili mambo na majukumu yake kutoka kwa Hazina ya Dola, (Bait ul-Mal). Ili dola itekeleze jukumu lililo wekwa mabegani mwake na Shari'ah, Shari'ah imeipa Dola mamlaka ya kukusanya mapato fulani. Sheikh Ata' bin Khalil Abu Rashtah anaeleza katika kitabu chake, Migogoro ya Kiuchumi, yafuatayo: "Mapato ya kudumu ya Bait ul-Mal "ngawira zote za kivita, jizya (kodi ya raia wasiokuwa Waislamu), kodi za ardhi (ushr, kharaj), khumus ya rikaz (mali iliyofichwa chini ya ardhi), mali za Dola, pamoja na ushuru wa forodha unaochukuliwa kutoka kwa wanaovuka mipakani na tulio na vita nao, fedha zinazotokana na mali ya Ummah, fedha za urathi wa wale wasiokuwa na warathi, fedha za ghushi zilizo nyang'anywa magavana na maafisa wa Dola, fedha zilizo chumwa kwa haramu, fedha za faini, fedha za walioritadi, na kodi…"

•* Fedha za Bait ul-Mal kimsingi zinatosha zaidi ya sana kukidhi majukumu yote haya. Dalili za Kiislamu zinaashiria waziwazi, kuwa utozaji ushuru kwa mujibu wa maana ya Kimagharibi ya neno "ushuru" ni haramu. Kwani Rasulullah (saw) amesema,

«إِنَّ صَاحِبَ الْمَكْسِ فِي النَّارِ»

"Hakika mtoza ushuru yuko Motoni."

Na yeye (saw) amesema

«إِنّ دِمَاءَكُمْ وَأَمْوَالَكُم وَأَعْرَاضَكُمْ عَلَيْكُمْ حَرَامٌ كَحُرْمَةِ يَوْمِكُمْ هَذَا فِي بَلَدِكُمْ هَذَا فِي شَهْرِكُمْ هَذَا... »

"Hakika damu zenu, na mali zenu na heshima zenu ni tukufu kama ulivyo utukufu wa siku yenu hii katika mji wenu huu katika mwezi wenu huu..."

Dalili hizi na nyingi zaidi zaeleza waziwazi kuwa Shari'ah imeharamisha utawala kutoza ushuru juu ya Waislamu. Uharamu huu unakusanya kila ushuru, uwe ushuru wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja, ada za mahakama, au vitengo, au mihuri ya uagizaji bidhaa, au ushuru wa forodha, au ada za leseni, au chochote mfano wake. Dalili hizi juu ya kadhia hii zimeelezewa kwa ufafanuzi katika Kielelezo cha Katiba au Dalili Zake Muhimu.

* Ni haramu kwa Dola ya Kiislamu kuchukua chochote kutoka kwa Ummah ambacho sio wajib juu yao, hata kutoka katika utajiri wao wa ziada! Hata kama hakuna chochote kilicho bakia katika Hazina, Dola inaruhusiwa pekee kuomba kutoka katika utajiri wa ziada wa matajiri miongoni mwa Ummah, na kisha kwa jukumu lililo faradhishwa na Shari'ah juu ya Ummah na Bait ul-Mal. Na wakati huo pekee, ambapo hakuna chochote kilicho bakia katika Hazina ya Dola, Dola inaruhusiwa kuchukua kiwango kinacho hitajika na Bait ul-Mal na wala si zaidi ya hicho. Hivyo kabla ya kuwaomba matajiri miongoni mwa Ummah usaidizi wao, Dola ni lazima itumie kila dirham katika Bait ul-Mal…

Ali (ra) alipendekeza kwa Umar Bin al-Khattab (ra) kusibakie chochote katika Bait ul-Mal akimwambia: "Ugawanye utajiri unaoupata kila mwaka, na usizuie chochote kutokana nao" (imeripotiwa na Ibn Sa'ad kutoka kwa al-Waqidi). Na imeripotiwa: "kuwa Ali alikuwa akitumia kila kitu katika Bait ul-Mal kufikia hadi angeifagia na kukaa ndani yake" (imeripotiwa na Ibn Abd al-Barrin Al-Istidhkar kutoka kwa Anas b. Sirin). (Muqaddimat).

* Hizb ut Tahrir inaeleza katika Kielelezo chake cha Katiba ya Dola ya Khilafah:
Kifungu cha 147: "Dola ina haki ya kutoza ushuru ili kutekeleza lolote ambalo Shari'ah imewajibisha juu ya Ummah endapo fedha katika Bait ul-Mal zitakuwa hazitoshi kwani uwajibu wa kulifadhili utagura kwa Ummah. Dola haina haki ya kutoza ushuru kwa ajili ya lolote ambalo si wajib juu ya Ummah kulitekeleza, na hivyo hairuhusiwi kukusanya ada za mahakama au vitengo au kutimiza huduma yoyote."
Sheikh Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah anafafanua waziwazi na kwa mkazo katika kitabu chake pamoja na Jibu la Swali (Tarehe: 19/05/2016 M) "wakati ambapo" Dola inaruhusiwa kutoza ushuru juu ya Ummah:

"Hivyo basi, utozaji ushuru katika Uislamu unahitaji kutimiza masharti mawili ili kuruhusu utozaji wake kwa ajili ya kutekeleza miradi, na kwa kiwango kilicho na umuhimu pekee:

1 – Mradi ni sharti uwe umewajibishwa juu ya bait ul-mal, yaani juu ya Dola na Waislamu, na uwajibu wake ni lazima uwe umepatikana kupitia nasi ya Kisheria. Hii ni mithili ya barabara muhimu, ambayo hakuna badala yake, au hospitali, wakati ambapo hakuna badala yake katika eneo, au viwanda vizito vya mashini au mifano yake ambayo kukosekana wake husababisha madhara kwa taifa, kutokana na Hadith ya Mtume (saw): رارض الو ررض ال» » "Hakuna kujidhuru wala kudhuru wengine."

2 – Ni sharti kuwe hakuna fedha za kutosha katika bait ul-mal. Ikiwa masharti yote haya hayatapatikana, hairuhusiwi kutoza ushuru, ikiwa mradi umewajibishwa juu ya Dola pekee kama

*Endelea Uk..9*

njia ya utekelezaji mambo ya kawaida ya watu, kama vile ujenzi wa barabara isiyo muhimu, au ujenzi wa hospitali ya pili mahali ambako tayari kuna hospitali; katika hali hii fedha hutumiwa juu yake kutoka kwa bait ul-mal endapo zitapatikana. Vilevile, ikiwa mradi umewajibishwa juu ya Waislamu, lakini kuna fedha za kutosha, hapo mradi huo hutekelezwa kutokana na fedha hizo pasi na kutoza ushuru.

Lakini, kama ilivyo tajwa mwanzoni kabisa mwa Makala haya, kuna baadhi ya aina za ushuru zilizowekwa na Shari'ah, kama Jizyah, Ushr na Kharaj, ambazo zitakusanywa na Khilafah kwa mujibu wa dalili katika Uislamu. Hizb ut Tahrir pia imedhibiti kadhia hizi katika Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah:

Kifungu cha 144: "Jizya hukusanywa kutoka kwa raia wasiokuwa Waislamu (watu wa Dhimma). Inatakiwa kuchukuliwa kutoka kwa wanaume walio baleghe ikiwa wana uwezo wa kulipa, na haichukuliwa kutoka kwa wanawake au watoto."

Kifungu cha 145: "Kodi ya ardhi hulipwa juu ya ardhi ya Kharaji kwa mujibu wa kiwango chake. Zakah hukusanywa kutoka kwa ardhi ya Ushri kwa mujibu wa uzalishaji halisi."

Kifungu cha 149: mapato ya kudumu ya Bait ul-Mal ni: ngawira (fei'), jizyah, kharaaj, khumus ya hazina iliyofichwa ardhini (rikaz) na zakah. Mali zote hizi hukusanywa, ima ziwe zahitajika au la, kwa msingi wa kuendelea."

Dalili ya hizi zimefafanuliwa katika Kielelezo cha Katiba au Dalili Zake Muhimu – Sehemu ya 2:

•*Kharaj huchukuliwa kama badala ya matumizi, kwa mujibu wa uwezo ardhi iliyo nao, na hiki si kiwango maalum. Kuna mambo kadhaa ambayo yanapaswa kuzingatiwa wakati wa kuamua kiwango cha Kharaj juu ya ardhi, au juu ya mimea au matunda yatokayo katika ardhi hiyo. Hivyo basi; rutba ya ardhi, ubora na idadi ya mavuno/mazao, mbinu za unyunyiziaji maji (mvua, visima, mikondo, mito, vinyunyizio, mashini nk), eneo la miundombinu na viunganishi, nk. yote ni mambo yanayo paswa kuzingatiwa ili kulinda ardhi pamoja na wakulima wake kutokana na madhara au utumizi wa kupita kiasi. Pia Rasulullah (saw) aliamrisha kuzingatia uzito wowote kwa wamiliki wa ardhi kupitia majanga ya kimaumbile na uharibifu wa mimea: "Punguzeni tathmini kwani katika mali kuna urathi, anaye athiriwa na hali ya baridi ya anga (Ariyyah), kukauka kwa mimea na majanga ya kimaumbile."

Khalifah Umar b. al-Khattab alimuuliza Uthman b. Haneef na Hudhayfah b. al-Yaman baada ya kurudi kutoka katika kuitafiti ardhi na kuweka kiwango cha Kharaj nchini Iraq (As-Sawad), kuhusu vipi wameweka kiwango cha Kharaj juu ya ardhi hiyo? Na kuongeza: "Huenda mumewabebesha mzigo watu mulio fanya kazi nao kwa lile ambalo hawawezi kulihimili?" Hudhayfah alisema: "Nimewacha baadhi ya ziada." Na Uthman akasema: "Nimewaacha walio madhaifu, lau ningetaka ningechukua kutoka kwao." (Mali katika Dola ya Khilafah na Sheikh Abdul Qadeem Zalloum). Kuna ufafanuzi mpana uliofafanuliwa katika vitabu vya Hizb ut Tahrir. Waweza kuvifikia katika linki niliyoiweka mwisho wa Makala haya …

•*Khilafah haitatoza chochote juu ya raia wake, wawe Waislamu au Dhimmi ambacho hawawezi kukimudu. Khalifah Umar (ra) aliharamisha unyanyasaji wa Dhimmi, ambao hawana uwezo wa kulipa Jizya. Alisema: "Waacheni na wala msiwatoze juu yao kile wasicho kimudu, kwani hakika nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akisema: «لَا تُعَذِّبُوا النَّاسَ، فَإِنَّ الَّذِينَ يُعَذِّبُونَ النَّاسَ فِي الدُّنْيَا يُعَذِّبهُمُ اللهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ» "Msiwaadhibu watu kwani hakika ya wale wanaowaadhibu watu duniani Mwenyezi Mungu atawaadhibu Siku ya Kiyama.'' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alimteua Abdullah b. Arqam juu ya Jizya ya watu wa Dhimma na akasema: «أَلَا مَنْ ظَلَمَ مُعَاهِداً، أَوْ كَلَّفَهُ فَوْقَ طَاقَتِهِ، أَوِ انْتَقَصَهُ، أَوْ أَخَذَ مِنْهُ شَيْئاً بِغَيْرِ طِيبِ نَفْسِهِ، فَأَنَا حَجِيجُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ» "Hakika, yeyote mwenye kumdhulumu mtu aliye chini ya mkataba (Mu'ahad), au akamkalifisha juu ya uwezo wake, au akamfedhehi, au akamnyang'anya kitu bila ya ridhaa ya nafsi yake, basi mimi nitakuwa mtetezi wake Siku ya Kiyama." (Mali katika Dola ya Khilafah)

Huu ndiyo uadilifu katika Nidhamu ya Kiuchumi ya Kiislamu. Khilafah inashikamana na maagizo ya Mwenyezi Mungu (swt), hivyo basi hupata mali zake kwa uadilifu na kwa wingi bila ya kumnyanyasa hata mtu mmoja, mazingira au kiumbe chochote chenye uhai au kisicho kuwa na uhai. Hili ndilo linalo hakikisha kuwa kila chenye uhai chini ya usimamizi wake daima hukidhiwa mahitaji yake yote.

**Zehra Malik**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vipi Khilafah Itakavyo Andaa Jeshi Lenye Nguvu Duniani Litakalo Pambana kwa Ajili ya Uislamu



• Tangu kuvunjwa kwa Khilafah 1924, usalama umekosekana ndani ya ulimwengu wa Waislamu, na kuwapelekea Waislamu kukosa mlinzi dhidi ya uvamizi wa madola ya kiulimwengu na kimaeneo, mapambano baina ya Waislamu yaliyo dhaminiwa kutoka nje na mabomu ya droni na kupelekea damu za Waislamu kukosa thamani. Fauka ya hayo, kuwepo kwa mashirika ya kiusalama ndani ya ardhi za Waislamu na matumizi ya majeshi ndani ya ardhi za Waislamu kupambana na watu wao inaonyesha wazi namna watawala walioko mamlakani hivi sasa ndani ya ulimwengu wa Waislamu walivyo telekeza jukumu la kulinda maisha ya watu wao wa kawaida.

• Mtume (saw) – alimuita Khalifah “ngao” na ni kurudi kwa ngao hii pekee ndiko kutakako pelekea kupatikana kwa amani na usalama ndani ya mipaka yake na kuwa lengo kuu la dola kwa mara nyingine.

“Siasa ni kusimamia mambo ya Ummah kindani na nje. Hutekelezwa na Dola na Ummah. Dola ndiyo husimamia mambo ya Ummah kivitendo moja kwa moja na Ummah unaihesabu Dola.” (Kifungu 181, Kielelezo cha Katiba, Hizb ut Tahrir)

• Usimamizi wa mambo ya Ummah kindani na kinje unatekelezwa kupitia utabikishaji wa mfumo (Uislamu). Kusimamia mambo ya Ummah kinje kunajumuisha mahusiano yake na dola nyingine, watu na Ummah nyingine na ulinganizi wa mfumo wa Kiislamu kwa ulimwengu hii ikiwa ndiyo sera ya kigeni ya dola ya Khilafah. Msingi wa sera ya kigeni ya Kiislamu umefungwa juu ya fikra isiyobadilika na inajumuisha kulingania ujumbe wa Uislamu kwa kila mtu na kila Ummah. Kwani Mwenyezi Mungu (swt) amesema:

يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ وَإِن لَّمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ

“Ewe Mtume! Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake.” [Al-Ma’idah: 67]

“Mwenyezi Mungu (swt) amewapa utukufu Waislamu kwa kuwafanya kuwa ndio walinganizi wa Ujumbe wa Uislamu kwa ulimwengu wote na Yeye (swt) na amewawekea njia ya kuubeba ulinganizi huo kwa Da’wah na Jihadi.” (‘Jeshi’, Nidhamu ya Utawala ya Kiislamu, Taqiuddin an-Nabhani, Hizb ut Tahrir)

• Ummah wa Kiislamu ni Ummah wa Jihadi na umefaradhishiwa kuulingania Uislamu kwa wanadamu wote.

Umepewa sifa ya Ummah ambao unaondosha udhalimu na ukandamizaji kutoka shingoni mwa watu.

• Kuulingania Uislamu duniani ni kitendo msingi cha kisiasa, lakini nguvu za kijeshi huchangia katika mchakato huo. Hivyo basi, Khilafah italenga kuwa na jeshi bora duniani ili kuiwezesha Khilafah kudumisha amani na usalama ndani ya Dar ul-Islam na kufungua ardhi za Ukafiri na kuwa za Kiislamu.

• Khalifah ndiye aliye na mamlaka ya kisiasa na kijeshi. Hivyo basi, ataliandaa jeshi kuwa imara ili kuweza kutimiza jukumu lake la Jihadi na kuulinda Ummah kutokana na uadui wa dola zisizokuwa za Kiislamu.

“Khalifah ndiye Amiri Jeshi na humchagua kiongozi wa maafisa wakuu, jemedari wa kila bendera kubwa na kiongozi wa kila kikosi.” (Kifungu 65, Kielelezo cha Katiba, Hizb ut Tahrir)

• Ujenzi wa sera ya kigeni ya Khilafah itatilia maanani dhurufu zote za hali ya kimataifa. Uislamu umeweka muongozo katika hili na vipi kuendesha mahusiano yake na dola zilizopo duniani

*Endelea Uk..11*

na kwa msingi huo Khilafah itachora mipango yake ya kisiasa ili kufikia malengo yake. La muhimu ni kwamba “njia muhimu zaidi ya kisiasa ni kudhihirisha utukufu wa fikra za Kiislamu katika kusimamia mambo ya watu binafsi, Ummah na dola.” (Kifungu 186, Kielelezo cha Katiba, Hizb ut Tahrir).

• Punde tu itakaposimama Khilafah, Khalifah atafanya kazi ya kusitisha mipaka baina ya Waislamu, kuziunganisha ardhi za Waislamu kuwa dola moja na kusimamisha jeshi moja. Miongoni mwa vipaombele itakuwa ni kuliboresha jeshi kwa thaqafa ya Kiislamu na kulipa dori yake ya kutumikia Uislamu na Waislamu.

• Khalifah binafsi atasimamia masuala ya jeshi na kubuni uhusiano baina ya ruwaza ya kisiasa na mipango ya kijeshi. Fauka ya hayo, kwa kuwa ni mwanasiasa na kiongozi wa kisiasa, Khalifah hafungwi na mtizamo finyu wa fikra za kijeshi na atabuni mbinu za kisiasa kushabiana na uwezo wa kijeshi ili kufikia malengo.

• Mafunzo ya kijeshi yataliboresha jeshi kwa ujuzi muhimu ili kutekeleza majukumu yake na kulipekea kuwa na taaluma ya kijeshi na ufahamu wa Kiislamu. Ufahamu wa Kiislamu ni muhimu mno katika kushajiisha vitani na kuimarisha ushindi kwa kuwavutia watu ambao ardhi zao zimefunguliwa upya ili waingie katika Uislamu na haki zake.

“Ni lazima jeshi lipewe elimu ya kijeshi ya ustawi wa juu zaidi inayowezekana, na kunyanyuliwa ustawi wake wa kifikra kadri inavyowezekana. Kila mtu katika jeshi lazima apewe thaqafa ya Kiislamu inayo muwezesha kuwa na busara ya kijumla kuhusu Uislamu.” (Kifungu 67, Kielelezo cha Katiba, Hizb ut Tahrir)

• Ni faradhi kulikabidhi Jeshi silaha, zana, vifaa na kila ambacho ni muhimu na kinachohitajika ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake kama jeshi la Kiislamu.

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ وَآخَرِينَ مِنْ دُونِهِمْ لاَ تَعْلَمُونَهُمُ اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ

“Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo, na kwa farasi walio fungwa tayari-tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, na wengineo ambao hamuwajui, lakini Mwenyezi Mungu anawaju.” [Al-Anfal: 60]

• Ni faradhi kwa kila kambi iwe na idadi ya kutosha ya maafisa wa ngazi za juu walio na taaluma ya kijeshi na tajriba ya kuchora mipango na kuendesha vita. Jeshi kwa ujumla lazima liwe na maafisa wengi iwezekanavyo.

• Kila mwanamume Muislamu ambaye ametimia umri wa miaka 15 ni faradhi kupata mafunzo ya kijeshi ili kuandaliwa kwa Jihadi.

• Mshahara wa jeshi lazima uendane na thamani iliyowekwa juu yake na Uislamu kwa kuwa na jeshi lenye uwezo na taaluma ya kijeshi. Mchakato wa kuchagua maafisa na wanajeshi lazima uhakikishe ni kwa watu bora walio na uwezo wa kazi hiyo. Mapendeleo hayato ruhusiwa kudhoofisha jeshi la Dola ya Kiislamu.

• Jeshi halito husishwa na siasa, biashara au chochote kuhusiana na idara za Serikali ambacho italipelekea kutotimiza majumu yake.

“Jeshi ni sehemu mbili: Sehemu ya Akiba nao ni Waislamu wote wanaoweza kubeba silaha, na Sehemu ya Daima wanaolipwa mishahara kutoka katika bajeti ya Dola kama wafanyikazi.” (Kifungu 63, Kielelezo cha Katiba, Hizb ut Tahrir) Kando na kubuni kuwa na jeshi lenye nguvu la Kiislamu lililopata thaqafa, sera ya kigeni itahakikisha kuna kuweko maumbile huru ya Khilafah na jeshi lake kwa:

• Kusitisha utegemezi wote wa kiteknolojia kutoka kwa dola adui kwa kubuni mpangilio kabambe na wakasi wa kiviwanda ili kufikia ubora wa kijeshi unaodhaminiwa na nidhamu bora ya kiuchumi inayozalisha mapato makubwa ili kuweza kutekeleza majukumu yote ya serikali ya Khilafah.

• Kusitisha mafunzo yote yanayo tegemea dola adui kwa kubuni taasisi za dola za kutoa mafunzo na mipango ya kijeshi na ufahamu wa Kiislamu.

• Kusitisha mahusiano yote na maafisa wa dola adui na yote yanayotokana na mahusiano hayo mfano mafunzo ya kijeshi kutoka ng’ambo, kubadilishana ujasusi na mahusiano ya jeshi kwa jeshi.

• Kuzitizama dola zote zisizokuwa za Kiislamu kwa mtizamo wa kivita. Haya ni mataifa ambayo yanakalia Ardhi za Waislamu au zimefanya vitendo vya kimabavu. Khilafah itazifunga rasilimali za Ummah kukomboa Ardhi zilizo vamiwa mfano Kashmir na Palestina.

• Kuondosha vitisho kutoka kwa dola adui kwa kusitisha kambi zao zote, balozi zao zote na watu wao wote ndani ya Ardhi za Waislamu.

• Kufutilia mbali mawasiliano yote ya kisiasa na kijeshi na dola adui ambazo zinatumia mawasiliano hayo kutoa maagizo na kuwakanya vibaraka wao ndani ya uongozi wa kijeshi na kisiasa na kisha kutafuta wapya. Yote haya yataiwezesha Khilafah kulinda ardhi zake, raia wake na wale Waumini ambao wanakandamizwa pamoja na kueneza haki na huruma ya Uislamu kwa mataifa duniani.

Mwenyezi Mungu (swt) asema:


وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلاَّ رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ

“Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.” [Al-Anbiya: 107]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Hizb ut Tahrir na**

**Yasmin Malik**

# Vipi Khilafah Italinda Uislamu na Ummah wa Kiislamu



Tangu Makafiri walipovunja Khilafah Ottomaniya kwa mikono ya Mustafa Kamal, vibaraka Waingereza tangu kubuniwa kwao miaka 94 miladia iliyopita, Ummah wa Kiislamu haujaona zuri lolote isipokuwa kuwa nyuma ya mataifa, ukiishi chini ya hali halisi iliyojaa machungu na fedheha, udhaifu na utumwa. Unaishi chini ya muongozo wa kikafiri na wanaopigia debe ukafiri. Na unaendelea kula makombo kutoka katika meza za dunia huku ukiendelea kulizwa na mataifa yote kutoka Mashariki na Magharibi. Kupoteza cheo chetu ambacho dunia ilikuwa inakiogopa na kupoteza Palestina, Iraq na mengineyo na kutawala kwa Ukafiri juu Waislamu kila mahali kama ilivyo Palestina, Syria, Mashariki Turkistan, Myanmar na nchi nyingine za Waislamu na kuenea kwa umasikini, njaa, ukosefu wa ajira, kudidimia kwa thamani, maadili na kubakia nyuma kisayansi na kiuchumi… yote ni natija ya kukosekana kwa Khilafah.

Kufikiria na thaqafa ya Kimagharibi kuanzia demokrasia, urasilimali, usekula na uhuru; unadhibiti nyanja zote za maisha na nidhamu za serikali, utungaji sheria, uchumi na utajiri, mtaala wa elimu na vyombo vya habari na mwenendo wa maisha. Kwa maana nyingine, nchi za Waislamu ziko chini ya ukoloni Umagharibi katika kila aina zake, kifikra, kisiasa, kiuchumi na kijeshi ndani ya nchi nyingi.

Machungu ya Ummah wa Waislamu yanayotokana na hali duni yasingelikuwepo lau kungelikuwepo na nguvu ya kuyasitisha au kuyapinga. Nguvu hii inayotishia inaweza kuwa kubwa, ya dhati na yenye nguvu inayotoka ndani ya Ummah; nidhamu yenye nguvu ambayo itakayositisha ukandamizaji na maonevu kwa kuikata mikono na kuyaondosha mamlaka yenye kufanya hivyo. Na nidhamu hii inatokana na itikadi ya Kiislamu ambayo imekuja kwa wahyi ambao tunaamrishwa kuifuata. Kuiwacha inatizamwa kuwa ni udikteta na kurudia nyingine katika kuhukumu ni Ukafiri, kukiuka na ukosefu wa haki. Kuhusiana na udikteta tunaamrishwa tuukufuru ima ni wa kihukumu zinazo husiana na mwanadamu kama mtu binafsi, kama hukm za swala, saumu au zinazo husiana na Ummah kama kikundi ambazo zinatekelezwa kupitia dola mfano nidhamu ya kuadhibu, muamalat, mahakama, uchumi, kijamii, elimu, sera za ndani na nje, makubaliano, vita, kuamrisha mema na kukataza maovu na mengineyo. Yote haya yanaweza kujumuishwa chini ya nidhamu ya dola ya Kiislamu, Khilafah. Hivyo basi, ni kimaumbile kusema kuwa kusimamisha dola hii ni kusimamisha hukm za Uislamu katika ardhi; ni mama wa faradhi zote na ni jukumu nambari moja la kufanya kazi kuisimamisha.

Lakini fikra kuhusu Khilafah ni ngeni na watu wamefahamu kuwa "kurudia Uislamu" ni kurudia katika ibada na akhlaqi za kibinafsi. Fikra za ujamaa, utaifa na uzalendo zilikuwa zenye mvuto sana wakati wa nyuma. Ilidaiwa kuwa Uislamu uko nyuma na ni ndoto isiyoweza kuwa kweli. Lakini shukrani ni kwa Mwenyezi Mungu (swt) na kufaulu ni Kwake kutokana na kazi ya mukhlisina ndani ya Ummah Wake, Khilafah na umoja wa Ummah chini ya mamlaka ya mtawala anayetawala kwa sheria za Mwenyezi Mungu imekuwa ndio mwito wa Waislamu katika ardhi hii na, licha ya kutofautiana katika njia na baadhi wamepotea njia kutoka ya sawa. Hivyo basi, Khilafah ni moja ya malengo makubwa ya Uislamu na sura kubwa ya umoja na

*Endelea Uk..13*

ushikamano unaoamrishwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَإِنَّ هَٰذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَٰحِدَةً وَأَنَا۠ رَبُّكُمْ فَٱتَّقُونِ

"Na kwa yakini huu Ummah wenu ni Ummah mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi, basi nicheni Mimi." [Al-Mu'minun: 52]

Kinachoonyesha kiu ya Ummah kutaka Uislamu ni kwamba kila mahali ambapo Waislamu wanatakiwa kupendekeza au kuchagua baina ya ambacho ni cha "Kiislamu" na chengine, katika umoja, miungano au taasisi au nyinginezo mshindi ni ile ya "Kiislamu." Yaliyotokea Tunisia, Misri, Jordan na kwengineko ni ushahidi wa hayo. Wanaoneysha muamko wa Kiislamu ambao unawafanya makafiri Wamagharibi kutetema kwa uoga wa kurudi kwa Uislamu katika ulingo wa mzozo wa kimataifa. Ulianza kupambana na Waislamu kama "wenye misimamo mikali, magaidi na wenye siasa kali."

Ni kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kuona kwamba sura ya Khilafah inaonekana zaidi kuliko hapo awali. Idadi kubwa wanataka na wanafanya kazi kurudisha utukufu wao wa zamani. Wanamuota Omar al-Farouq, Omar bin Abdul-Aziz, Salah ud-Din al-Ayyubi, Saqr Quraish, Harun ar-Rashid... nk. Wanatamani izza, hadhi, haki na nguvu mpaka warudi wawe Ummah bora uliotolewa kwa watu.

Dola hii ya Kiislamu iliyoahidiwa –Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume – ni dola ya kimfumo ambayo katiba yake imetokana na itikadi ya Kiislamu na Waislamu wamepewa amana ya kuifikisha itikadi hii kwa watu na mataifa yote.

Lau tutaangalia yale ambayo dola ya Khilafah inaweza kufanyia Uislamu na Ummah wa Kiislamu, tutaona ndani ya nyanja zote za maisha:

Utawala kwa mujibu wa sheria za Mwenyezi Mungu utarudi, na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah ya Mtume wake (saw) utarudi kuwa ndio marudio ya Ummah kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu (swt):

وَأَنِ احْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ وَاحْذَرْهُمْ أَنْ يَفْتِنُوكَ عَنْ بَعْضِ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ إِلَيْكَ

"Na wahukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao. Nawe tahadhari nao wasije kukufitini ukaacha baadhi ya aliyo kuteremshia Mwenyezi Mungu." [Al-Ma'ida: 49].

Imamu, mtawala muadilifu atarudi na kundi litaungana baada ya kugawanywa na Ummah utarudi kuwa Ummah mmoja na mwili mmoja baada ya wakoloni kuugawanya na kuufanya kuwa vijidola vingi na makabila mengi. Mtume (saw) asema: «إِنَّمَا يَأْكُلُ الذِّئْبُ مِنَ الْغَنَمِ الْقَاصِيَةَ» "...Hakika mbwa mwitu humla mnyama aliyepotea."

Twasema kuwa ni wangapi waliopotea wameliwa tokea kuvunjwa kwa Khilafah; Palestina, Iraq, Kashmir na Mashariki Turkistan wote wamepotea na orodha inaendelea. Wote watakuwa dola moja bila mipaka wala vizuizi na fungamano la kiitikadi litakuwa ndio msingi na kuondosha mafungamano ya uzalendo, utaifa na mafungamano yanayo dorora. Uwiano wa jamii, watu na dola utazidi.

Kwa kurudi kwa Khilafah, ni kurudi kwa usalama na amani na nguvu za Waislamu na cheo chake cha kuogopewa ndani ya mioyo ya maadui zao. Cheo hichi cha kuogopewa kilipotea kwa kupotea Khilafah. Mwenyezi Mungu alikiondosha cheo cha kuogopwa kutoka katika mioyo ya maadui zetu kwa mujibu wa maneno ya Mtume (saw):

وَلَيَنْزِعَنَّ اللهُ مِنْ قُلُوبِ أَعْدَائِكُمُ الْمَهَابَةَ مِنْكُمْ

"na Mwenyezi Mungu ataondosha uoga kutoka katika vifua vya maadui zenu wasiwaogope."

Moja kati yao, hususan watawala wamekuwa kama watumwa. Anaposhambuliwa kimaneno au kimwili na bwana wake, hawezi kufanya lolote na cheo cha kuogopwa na kutishiwa na adui kutarudi, Mtume (saw) anasema: «نُصِرْتُ بِالرُّعْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ» "Mwenyezi Mungu amenipa ushindi kwa kuwaogopesha maadui zangu kwa urefu wa safari ya mwezi mmoja." na «الإِسْلامُ يَعْلُو وَلا يُعْلَى عَلَيْهِ» "Uislamu daima uko juu na hautakiwi kupitwa."

Imamu, ni ngao ambayo nyuma yake tunapigana itarudi, ambaye atatangaza Jihadi kueneza Uislamu duniani kote. Na atayaunganisha majeshi kuikomboa ardhi tukufu ya Palestina na kuirudisha katika moyo wa Uislamu na dola ya Kiislamu, ardhi ya Isra na Mi'raj, ardhi ya Mahsher and Mansher (kujumuika na kufufuliwa).

Umbile la Kiyahudi lisingelikuwepo katika ardhi ya Palestina lau Khilafah ingelikuwepo. Sote tunajua cheo cha Khilafah wakati wa Ottomaniya na kukataa kwao kuipoteza hata kama ilikuwa katika hali dhaifu. Imamu ataulinda Uislamu na Waislamu kila mahali na kujibu uadui na ukosefu wa haki na kuokoa maisha, pesa na majumba yao.

Utajiri wa Ummah wa Kiislamu, rasilimali na pesa zake zitarudishwa, ambazo zimeporwa na Makafiri na vibaraka wao mbele ya macho na masikio ya Waislamu. Uchumi wake utaimarika. Biashara, viwanda na ukulima, mahusiano ya kibiashara tofauti tofauti ndani na nje yatarudi. Khalifah atatumia rasilimali katika kusimamia mambo ya Ummah na maslahi yake ili watu waweze kuishi kwa hali nzuri, ustawi, baraka na furaha. Ibn Khaldun alitaja katika utangulizi wake kwamba yale yaliyopelekwa katika Bait ul-Mal (hazina) ya Waislamu ndani ya Baghdad wakati wa Khilafah ya Abbasiya ya al-Ma'mun ni sawa na dola bilioni 70 na tani 1,700 za dhahabu leo. Itakuwaje leo lau Waislamu wangelikuwa na Khilafah Rashida kwa njia ya Utume na Mwenyezi Mungu (swt) akawabariki na Khalifah mchamungu. Kutabakia nyumba ya Muislamu masikini?! Mwenyezi Mungu amuhurumie Khalifah muadilifu Umar bin Abdul Aziz ambaye chini ya Khilafah yake Waislamu hawakupata hata mtu mmoja anayestahiki Zaka.

Hukm za nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu zitatekelezwa na mabenki ya riba, ukiritimba, ukosefu wa ajira, mapendeleo na watu wa kati na kati wataondoka na kila mmoja aliye na haki ya kufanya kazi au kustahiki cheo atachukua.

Uislamu na Ummah wa Kiislamu utarudi tena katika ushindi wake na izza yake na kuchukua sehemu yake ya mbele ya kisayansi. Elimu itakuwepo katika kila ngazi na haitofungwa kwa matajiri na wenye nguvu. Dola itakuwa na uwezo wa kisayansi na kiteknolojia unaohitajika kwa viwanda vizito, vita vya kisasa na nyanja nyingine za maisha zitakazotumiwa katika ulinganizi wa Uislamu. Yote haya yatawezekana pale tu kutakapo kuwepo na Sultan (kiongozi) mchamungu, anayejali maslahi ya Ummah wake na haya ni kupitia kumiliki viwango vya juu vya kiteknolojia na wanasayansi wabunifu. Panapokuwa na dola ya Khilafah inayodhamini ubunifu, wasomi Waislamu ambao wamehamia Magharibi watarudi.

Endelea Uk..14

Upeo wa kisayansi na kijeshi utarudi kama ilivyokuwa zamani pale Waislamu walipoweza kushinda upeo wa kisayansi na kijeshi wa Roma na Fursi. Baada ya hilo Waislamu waliweza kuchimbua rasilimali katika ardhi hizo na kuvumbua sheria za kisayansi zinazo watawala na kufaulu kufikia viwango vya juu vya kiutabibu, uhandisi, falaki, maeneo na mengineyo. Ulaya ilituma wanafunzi wake kupokea sayansi kutoka kwa Waislamu.

Hukm za Mwenyezi Mungu na sheria za kuadhibu zitatekelezwa tena. Yeyote atakayekiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu ataadhibiwa. Makosa yanayo ficha fikra sahihi za Kiislamu yataondoka; kwani yametokana na Wamagharibi na wandani wao ambao wamebeba fikra zilizo oza za hadhara ya kisekula ya kirasilimali. Na muundo wa familia na wanawake utarudi katika sehemu yake iliyowekwa na Uislamu, ambayo iliondoshwa na maadui wa Uislamu waliovutiwa na thaqafa ya Kimagharibi na kumpotosha mwanamke kuwa ana haki ambazo Uislamu umemnyima, na kwamba eti amefaulu kupata yale ambayo Uislamu umemnyima, ilhali uhalisia ni kinyume chake; kudorora na majanga yanayomkumba mwanamke yanasababishwa na kukaa mbali na hukm za Uislamu na kubeba mtizamo wa Kimagharibi katika kutafuta haki zake.

Khilafah Rashida italinda hadhi ya Ummah na kuwalinda wanawake na italiongoza jeshi lake. Hivi ndivyo alivyo fanya Mtume (saw) pale ambapo mwanamume Myahudi alipo shambulia vazi la mwanamke Muislamu na ndivyo alivyo fanya Khalifah al-Mu’tasim. Khilafah Rashida ndiyo inayo linda familia na jamii kutokana na makosa na ufisadi na kutekeleza nidhamu ya kijamii na kuondosha uchafu na mchanganyiko. Itaondosha uovu na ukiukaji wa sheria za Mwenyezi Mungu na haki za watu. Khilafah itadhibiti vyombo vya habari na kuviongoza kwa maslahi ya Ummah, itafunga channeli na vipindi vya kifisadi na ufisadi na kufuatilia kwa karibu mitandao ya angavuni ili kuondosha mitandao mibaya kutoka kwa watu. Madhambi na sababu za ufisadi ni natija ya moja kwa moja ya kukosekana kwa umbile la kisiasa linalo tekeleza sheria ya Mwenyezi Mungu. Izza na ulinzi wa wanawake ni Khilafah, Khilafah ndio mlinzi. Vita vya Wamagharibi dhidi ya vazi la kiShari’ah na sheria za nidhamu ya kijamii ni vita dhidi ya Uislamu.
Baada ya yote haya, na kukosekana kwa muda mrefu kutekeleza sheria za Mwenyezi Mungu katika maisha yetu kwa kukosekana kwa dola ya Uislamu iliyo dhaminiwa na Khalifah wa Waislamu na mamlaka yao. Kwani haujafikia wakati ambapo Waislamu warudie kile ambacho kitawapa izza na chanzo cha nguvu zao na umoja wao. Baada ya kuona kwa macho yao namna madhambi yalivyo wapelekea kutaabika? Ni kuachana kwao na Dini na kuitelekeza katiba yao na hukm za kiShari’ah. Mwenyezi Mungu (swt), Msema Mkweli, asema:


**وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنكًا وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى * قَالَ رَبِّ لِمَ حَشَرْتَنِي أَعْمَى وَقَدْ كُنتُ بَصِيرًا * قَالَ كَذَلِكَ أَتَتْكَ آيَاتُنَا فَنَسِيتَهَا وَكَذَلِكَ الْيَوْمَ تُنسَى**

“Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu. Aseme: Ewe Mola wangu Mlezi umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona? (Mwenyezi Mungu) atasema: Ndivyo hivyo. Zilikufikia ishara zetu, nawe ukazisahau; na kadhalika leo unasahauliwa.” [Ta-Ha: 124-126]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Muslima Ash-Shami (Umm Suhaib)**

# Vipi Khilafah Itakavyo Sitisha Ukoloni ndani ya Ardhi za Waislamu



• Leo kuna zaidi ya dola hamsini za Waislamu, zote zikidai kuwa Uislamu ndio dini yao na chimbuko la utambulisho wao. Dola zote hizi daima ziko katika mchakato wa kujenga na kujenga upya matumaini ya kufaulu katika malengo ya maendeleo yaliyowekwa na Wamagharibi. Malengo haya yanakwenda kinyume na dini ambayo wengi wanatangaza kujifunga kwayo kama dini ya dola.

• Matatizo ya kimwili na kimali yametokana na kujitenga na kufanya ibada na kumepelekea maumivu ya kimwili, kiakili na kihisia kwa takribani wafuasi bilioni 1.8 wa Uislamu na hawatoweza kuondokana na hili mpaka pale ambapo tatizo linalo sababisha hayo ambalo ni kujisalimisha kwa mabwana wakoloni limeondoshwa kabisa.

• Dola za Waislamu ni wahanga wa ukoloni mambo leo ambao una nguvu lakini hauna majukumu, kwa kuwa ni aina mbaya ya ukoloni. Dola ya Khilafah itahakikisha kuwa hakuna serikali, mashirika, taasisi au wacheza dori kutoka nje wana uwezo wowote kuingilia kati kisiasa, kiuchumi, kijeshi au kielimu katika usimamizi wa mambo ya serikali. Itasitisha uchakachuaji wa uchumi wetu ili kuhudumia maslahi ya serikali za Kimagharibi na mashirika ya kigeni. Itakataa mikopo ya IMF na sera zake ambazo ndio chanzo cha kupunguza matumizi ya serikali katika afya, elimu na aina zote za ustawi na kupunguza thamani ya pesa za Waislamu zikilinganishwa na dolari ya Marekani. Dola ya Khilafah itatekeleza nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu ambayo haitotoa tu suluhisho la umaskini na kuganda kiuchumi katika ardhi za Waislamu bali pia itakuwa ni chanzo cha kulingania nidhamu ya Kiislamu kwa nchi za Ulimwengu wa Tatu ambazo zimetiwa kitanzi kutokana na sera kandamizaji za kirasilimali na mikopo ya riba. Pesa za Waislamu zitadhaminiwa kwa dhahabu na fedha kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu (swt). Hii itamaanisha kuwa fikra ya akiba ya sarafu itaanguka.

• Siasa ni kiungo muhimu katika kusimamisha serikali ya Kiislamu. Kuweko na hisia ya Kiislamu katika siasa ndani ya dola za kikoloni na zisizokuwa za kikoloni zimekuwa kikwazo kwa usekula kutochukua mamlaka kamili. Kuweko kwa makundi ya Kiislamu ni ushahidi tosha kuwa ndani ya mioyo watu wanajua kuwa suluhisho la matatizo yao lipo katika Uislamu. Qur'an na Sunnah ndio itakuwa chanzo cha sheria na chama chochote kitakachokuwa kinalingania chochote kinyume na Uislamu kitakataliwa na kushtakiwa.

Dola ya Khilafah itakuwa na dori ya kufichua sura mbaya ya ulafi wa siasa za kirasilimali ambayo umeipelekea dunia kuwa katika uwendawazimu uliopo sasa ambapo thamani ya maisha inapimwa kwa kutumia pesa na rangi. Nidhamu hii ya kidhalimu ya kisiasa inawatumia watu kama nguru wa kufanyiwa majaribio ya kimatibabu, kijamii au kiuchumi; itaondoshwa katika ardhi zote za Waislamu na hii itakuwa ni mfano mzuri kwa nchi nyingine na njia ya da'wah.

"Baadhi ya mbinu muhimu za kisiasa ni kufichua uhalifu wa dola nyingine, kuonyesha hatari ya siasa zao, kufichua madhara ya njama zao na kuvunjilia mbali utambulisho wao." (Kifungu 185, Kielelezo cha Katiba ya Hizb ut Tahrir kwa serikali ya Khilafah)

*Endelea Uk..16*

• Athari nyingine ya ukoloni ni utumwa wa kiakili katika watu. Huku fikra zao zikijaribiwa, uwezo wao ukifedheheshwa, elimu yao ikibandikizwa kuwa haina maana na ushujaa wao ukitajwa kuwa ni uhayawani na kuficha machungu yao eti ni kuiga kwa utiifu. Kurudi kwa Khilafah itakuwa ishara tosha kuwa akili imeanza kubadilika na mengine yatafanywa kutokana na mazingira yatakavyo kuwa yameandaliwa na Dola. Badala ya kukandamizwa, Waislamu watahisi kuthaminiwa na watacheza dori muhimu pasina kurudi nyuma katika itikadi yao. Serikali ya Khilafah itaandaa nidhamu ya elimu ambayo itatibu maradhi ya kukosa utulivu katika akili na kujenga kizazi cha Waislamu wa kweli. Serikali itang'oa ukoloni wa Kimagharibi katika kuingilia kati mtaala wa elimu ndani ya ardhi za Waislamu ambazo zimelenga kupandikiza fikra na utiifu wa Kimagharibi katika akili za vijana Waislamu na kuwafanya kuwa masekula na matamanio na hisio zao ni kwa mujibu wa uhuru. Lakini, Khilafah itatekeleza nidhamu ya kijamii ambayo imejengwa kutokana na Uislamu safi na inayolenga kujenga utambulisho (Shaksiyya) wa Kiislamu na akili bunifu na za uongozi katika kila nyanja ya maisha na masomo. Itaandaa kizazi ambacho kwa mara nyingine kitatoa kwa ulimwengu akili kama za Abd-al-Rahman al Sufi (aliyevumbua nidhamu ya nyota mbali zaidi ya Milky Way), Ibn Firnas (mtu wa kwanza kuruka angani), Fatima al Fihri (mwanamke wa kwanza kuzindua chuo kikuu), Al Zahrawi (mjuzi wa upasuaji). Hawa ni baadhi tu ya majina kutoka katika historia iliyojaa Waislamu waliofaulu na sababu ya kufaulu kwao ni kutokana na akili iliyojengwa na elimu ya Kiislamu.

"Lengo la sera ya elimu ni kuunda utambulisho wa Kiislamu kifkra na kitabia. Hivyo basi, masomo yote katika mtaala lazima yachaguliwe kwa msingi wa sera hii." (Kifungu 171, Kielelezo cha Katiba ya Hizb ut Tahrir kwa serikali ya Khilafah)

• Sera ya Kigeni ya Khilafah itakuwa Da'wah na Jihadi, Waislamu watalindwa na kueneza Uislamu. Ukoloni ndani ya ardhi za Waislamu ulianza tokea Muingereza na nchi za Ulaya zilipoingia katika ardhi za Waislamu na kupora rasilimali zao na kuua watu wao na wanaendelea kupora na kuua.

Khilafah itaondosha kambi za kijeshi, majeshi na majasusi wa kigeni kutoka katika ardhi yake na haitokubali kattu mmoja wa wanajeshi wake kutumika kama kibaraka ili kupigana kwa maslahi ya serikali za kigeni. Serikali ya Khilafah pia itasitisha mateso ya Waislamu katika nchi zisizokuwa za Kiislamu. Badala ya kuiomba Umoja wa Mataifa, Khilafah itaunganisha jeshi lake na kuwakomboa watu wa Rakhine, Kashmir, Palestina, Mashariki ya Turkistan na Syria. Viongozi Waislamu madhalimu kama Rais Sisi wa Misri na Muhammad Bin Salman wa Saudi Arabia lazima wahesabiwe kwa makosa ya kumwaga damu za Waislamu. Serikali zote za Waislamu zitajumuishwa kuwa chini ya dola moja ambayo ina nguvu na uwezo wa kuathiri hali ya kimataifa. Umoja na mamlaka pamoja na nguvu za kweli zitaifanya Khilafah kuwa kubwa kisiasa, kiuchumi na kijeshi na kuogopwa na makafiri wote. Chini ya Khilafah, Waislamu hawatopata tu ulinzi na usalama bali pia watajua maana ya kweli ya Jihadi. Jeshi lililoandaliwa kwa thaqafa ya Kiislamu ndio litakuwa uti wa mgongo wa serikali.

"Ni lazima jeshi lipewe elimu ya kijeshi ya ustawi wa juu inayowezekana, na kunyanyuliwa ustawi wake wa kifikra kadri iwezekanavyo; na kila mtu katika jeshi kupewa thaqafa ya Kiislamu inayomuwezesha kuwa na busara ya kijumla kuhusu Uislamu." (Kifungu 67, Kielelezo cha Katiba ya Hizb ut Tahrir kwa serikali ya Khilafah)

Enyi kaka na dada, sote tumechokana na mabaki yaliyo oza ya ukoloni. Wakati umetima wa kuyaondosha pamoja na wale wanaudhamini mfumo huu ulio oza. Umejaza dunia kwa machungu na mahangaiko na tiba iko katika kuikumbatia nguvu waliyopewa Waislamu na Mwenyezi Mungu (swt) – Kutekeleza nidhamu ya Mwenyezi Mungu (swt) katika mgongo wa ardhi hii.

وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقًا

"Na sema: "Kweli imefika, na uwongo umetoweka. Hakika uwongo lazima utoweke!" [Al-Isra: 81]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ikhlaq Jehan**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**


Email: info@uqab.or.ke